

Tathmini ya Usimamizi wa Rasilimali hupima ubora wa usimamizi katika sekta za mafuta, gesi, na uchimbaji wa madini. Kwa mwaka 2013, nchi 58 zilitathminiwa. Kwa taarifa zaidi za matokeo ya tathmini hii tembelea tovuti: www.revenuewatch.org/rgi.

Utangulizi (Usuli)

Uchimbaji madini huchangia asilimia 5 ya pato ghafi la ndani (GDP) na theluthi moja ya mauzo ya nje. Mwaka 2011 thamani ya mauzo ya nje ya madini ilifikia kiasi cha dola za marekani bilioni 2.1, kati ya hizo zaidi ya asilimia 95 zilitoka katika machimbo sita ya dhahabu. Tanzania pia inazalisha shaba, madini fedha, almasi, na gesi asilia.

Umuhimu wa sekta unakua kwani thamani ya mauzo ya nje ya madini imeongezeka karibu mara nane kati ya mwaka 2005 na 2010.

Tanzania	2000	2005	2011
Idadi ya watu (milioni)	34.04	38.83	46.22
Pato ghafi la ndani GDP (kwa thamani ya 2011 katika bilioni za \$)	13.0	16.0	23.9
Pato ghafi la ndani kwa kichwa, thamani ya \$ kwa wastani wa kimataifa mwaka 2005	868	1,070	1,336
Mauzo ya nje ya madini na gesi asilia (kama % ya Jumla ya mauzo nje ya nchi)	1%	12%	37%

CHANZO: Benki ya Dunia.

Matokeo ya Tathmini.

Tanzania ilipata alama hafifu ya asilimia 50, ikishika nafasi ya 27 kati ya nchi 58. Alama ya juu iliyopata katika kipengele cha Uthibiti na Usimamizi wa Ubora ilishushwa kwa kutokufanya vizuri katika vipengele vingine.


Hali ya Kitaasisi na ya Kisheria (Nafasi: 46 kati ya 58, Alama: 44 kati ya 100)

Alama "hafifu" ya Tanzania kwa upande mmoja inatokana na utoaji wa taarifa usiofikia viwango vinavyotakiwa na kutokuwepo sheria ya uhuru wa kupata habari.

Wizara ya Nishati na Madini na Mamlaka ya Mapato Tanzania hukusanya mapato kutoka makampuni ya madini. Makampuni hufanya baadhi ya malipo moja kwa moja kwa jamii/mamlaka za mitaa kwenye maeneo ya migodi, vinginevyo mapato yote hupelekwa hazina.

Baada ya miaka mingi ya makukusanyo kidogo sana ya mrabaha (malipo kwa kutumia ardhi yao) kutoka makampuni ya uchimbaji madini, Serikali ilipitia sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kuongeza viwango vya mrabaha kwa kati ya asilimia moja hadi mbili kutegemeana na aina ya madini, ingawaje makubaliano ya ki-mkatiba na makampuni hayo bado hayajawekwa wazi.

Tathmini ya athari za kimazingira inahitajika, lakini makampuni hawaitoi wakati wote kabla ya utoaji wa leseni, na kampuni ya taifa ya uchimbaji madini hailazimiki kuchapisha taarifa za mapato. Hata hivyo, Tanzania imejiunga na Mpango wa Uwazi katika tasnia ya uzidujaji (madini mafuta na gesi); mwezi Desemba 2012, Tanzania ilipitishwa na bodi ya kimataifa ya mpango huu baada ya kukidhi viwango vya uwazi kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na bodi hii.



Utaratibu wa Utoaji Taarifa

(Nafasi: 27 ya nchi 58, Alama: 48 ya nchi 100)

Wakati Tanzania inatoa baadhi ya taarifa kuhusu uzalishaji wa madini na mapato, kutoweza kuchapisha mikatiba ya uchimbaji madini na ukosefu wa taarifa / takwimu kuhusu kampuni ya taifa ya uchimbaji madini ilipelekea katika kupata, "alama hafifu".

Taarifa chache sana zinapatikana kuhusu utaratibu wa utoaji leseni kabla leseni hazijatolewa. Mara hati za kuruhusu uchimbaji zinapotolewa taarifa zinakuwepo katika maelezo ya kitakwimu ambayo ni magumu kueleweka na hupatikana baada ya kutoa ada / malipo, na tathmini ya athari za kimazingira hupatikana tu baada ya kuomba upewe.

Wizara ya Fedha huchapisha taarifa kuhusu viwango vya uzalishaji na thamani ya mauzo ya nje, lakini haitoi takwimu za mapato. Wizara ya Nishati na Madini huchapisha taarifa kuhusu akiba, viwango vya uzalishaji, bel, thamani ya mauzo ya nje, makampuni yanayoendesha shughuli, kodi na mrabaha, lakini bado haijaweka wazi takwimu kuhusu malipo ya leseni, malipo kwa ekari, gawio au bonasi (malipo ya ziada) Benki ya Tanzania huchapisha taarifa za mwaka kuhusu mauzo ya nje na viwango vya uzalishaji na thamani zake.

Udhibiti na Uhakiki wa Ubora

(Nafasi: 17 ya nchi 58, Alama: 68 ya nchi 100)

Tanzania ilipata alama ya juu zaidi katika kipengele hiki kuliko vipengele vingine, kutokana matakwa ya kisheria kwa viongozi kuweka wazi panapo kuwepo mgongano wa kimaslahi na uhakiki/ufuatiliaji wa kuridhisha katika mchakato wa uandaaaji wa bajeti na matumizi ya fedha za umma kupitia kamati za bunge).

Lakini, sheria mpya haijaondoa mamlaka ya waziri mwenye dhamana ya nishati na madini katika maamuzi yanayo husu utoaji wa leseni na majadiliano ya mikatiba. Sheria mpya ya uchimbaji madini haiweki wazi wajibu wa bunge ambalo kwa sasa, halifanyi mapitio ya mapato yanayotokana na uchimbaji madini kwa utaratibu mahsus.

Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania ulianzishwa Desemba 2009. Kwa ujumla uanzishwaji wake unachukuliwa kama hatua ya kimaendeleo na taarifa zake za mwaka zimeongeza upatikanaji wa taarifa kwa umma. Hata hivyo, uhuru wake ki-madaraka unatiliwa mashaka na baadhi ya asasi za kiraha kwani bado upo chini ya wizara ya nishati na mdini.

Mazingira Wezeshi

(Nafasi: 24 ya nchi 58, Alama: 42 ya nchi 100)

Tanzania ina mazingira wezeshi yaliyo "dhaifu" yenye alama za chini hasa katika ufanisi wa kiutendaji na utawala wa sheria. Ina alama za chini katika viashiria vya kupambana na rushwa na uwajibikaji.

Makampuni ya Umma

(Nafasi: 31 ya nchi 45, Alama: 33 ya nchi 100)

Kampuni ya Taifa ya Madini (STAMICO) inamilikiwa na serikali. Imekuwa haifanyi kazi kwa siku za karibuni, lakini Serikali ina matumaini ya kuiimarisha ili iweze kuendesha shughuli za kibiashara kwa ubia na makampuni binafsi. Mpaka sasa hivi STAMICO imeshiriki katika shughuli moja tu kwa ubia na hakuna taarifa zozote kuhusu shughuli za baadaye. Kampuni inakaguliwa kila mwaka lakini haichapishi taarifa kuhusu shughuli zake au mapato yake.

Mfuko wa Mali Asili na Uhaulishaji Mdogo wa Kitaifa

Serikali imetoa tamko la kuonesha kusudio la kuanzisha mfuko maaluma wa maendeleo ya madini, lakini hilo bado halijatokea. Viongozi wa asasi za kiraia wametetea hitaji la uhaulishaji (uhamishaji) mdogo wa wa mapato yatokanayo na uvunaji wa rasilimali; na makampuni ya uchimbaji madini hivi sasa hulipa \$ 200,000 moja kwa moja kwa serikali za mitaa katika maeneo wanakoendesha shughuli zao.

Alama za Viashirio kwa Vipengele Tofauti Tanzania

Nafasi (kati ya 58)	Alam (chini ya 100)
27 ALAMA KWA VIPENGELE TOFAUTI	50
46 Hali ya Kitaasisi nay a Kisheria	4
Sheria ya uhuru wa habari	0
Sheria yenye upeo mpana wa kisekta	67
Ushiriki wa EITI	67
Utaratibu wa utoaji leseni ulio huru	100
Tathmini ya athari za kimazingira na kijamii zinazohitajika	50
Uwazi katika ukusanyaji wa mapato	67
Usawa katika sekta pana ya umma	0
Taarifa za fedha zinazohitajika za MU	0
Kanuni za Mfuko zimewekwa kisheria	0
Kanuni za uhawilishaji mdogo kitaifa	0
27 Utaratibu wa Utoaji Taarifa	48
Taratibu za utoaji leseni	50
Mikataba	0
Tathmini zinazohitajika za athari za kimazingira na kijamii	50
Takwimu za utafutaji madini	50
Kiasi cha uzalishaji	100
Thamani ya uzalishaji	100
Vyanzo vikuu vya mapato	50
Vyanzo vingine vya mapato	100
Ruzuku	0
Majina ya makampuni yanayoshughulika	100
Taarifa pana ya Makampuni ya Umma	0
Takwimu za uzalishaji za Makampuni ya Umma	0
Takwimu za mapato za Makampuni ya Umma	0

Nafasi (kati ya 58)	Alam(chini ya 100)
Taarifa pana ya mfuko	
Kanuni za uhawilishaji mdogo kitaifa	
Taarifa pana za uhawilishaji mdogo kitaifa	
Taarifa za ndani kuhusu uhawilishaji	
51 Usalama na Ubora wa Thamani	68
Uthibiti katika taratibu za utoaji leseni	33
Uthibiti katika mchakato wa bajeti	89
Ubora wa taarifa za serikali	71
Uwekwaji wazi na serikali wa ukinzani wa kimaslahi	100
Ubora wa taarifa za makampuni ya umma	0
Taarifa za makampuni ya Umma zimekaguliwa	50
Utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utunzaji fedha na MU	100
Uwekwaji wazi na MU wa ukinzani wa kimaslahi	100
Ubora wa taarifa za mfuko	
.. Taarifa za mfuko zimekaguliwa	
.. Serikali inafuata kanuni za mfuko	
.. Uthibiti wa matumizi ya mfuko	
.. Uwekwaji wazi wa ukinzani wa kimaslahi na mfuko	
.. Ubora wa taarifa za uhawilishaji mdogo kitaifa	
.. Serikali kuzingatia kanuni za uhawilishaji mdogo kitaifa	
39 Mazingira Wezeshi	42
Rushwa (TI Kipimo cha hisia za rushwa &WGI uthibiti wa rushwa)	42
Bajeti ya Wazi (IBP Index)	48
Uwajibikaji&demokrasia (EIU Kipimo cha Demeokrasia & WGI sauti & uwajibikaji)	46
Ufanisi wa serikali (WGI)	38
Utawala wa sheria (WGI)	36
Shughuli za kifedha za Makampuni ya Umma	..
Wakurugenzi wa bodi wa Makampuni ya Umma	50
Kanuni za Mfuko	..

Inaridhisha Hafifu

Kiasi Imeshindwa

Policy Forum ni mtandao wa Asasi zaidi ya 100 za kiraia za Tanzania zilizoungana pamoja kwa dhamira ya kushawishi mchakato wa uundwaji sera ili kupunguza umaskini, kuleta usawa na demokrasia wakijikita zaidi katika uwajibikaji wa serikali kwa matumizi ya fedha za umma. www.policyforum.or.tz

Revenue Watch Institute (RWI) ni taasisi ya kisera inayosaidia nchi zenye utajiri wa madini, mafuta na gesi asilia kunufaika kimaendeleo na utajiri wa rasilimali zao. www.revenuewatch.org